

SHULE YA SEKONDARI MPESU,
S.L.P 6588,
MBEYA.
Barua pepe.....
Mob: 0763873323

Kumb. Na. MPESS/F.I.JI/VI/2021

15/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MPESU
WILAYA YA MBEYA MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.**

1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021 shule ya sekondari MPESU.

Muhula wa masomo utaanza mnamo tarehe 11/01/2021 unatakiwa shulenii kuanzia tarehe 11/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare ya shule

(a) Sare hii ni – **WAVULANA**

- Suruali mbili: (moja rangi ya dark blue na moja rangi ya blue bahari)
- Shati nyeupe mbili mikono mifupi
- Mkanda mweusi upana wa kawaida
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visivyo na kisigini kirefu pea mbili (2).
- Soksi pea nne rangi nyeupe
- Bukta kwa ajili ya michezo
- Sweta 2 rangi ya dark blue

(b) **WASICHANA**

- Sketi mbili ndefu mpaka chini (moja rangi ya dark bluu na nyingine rangi ya bluu bahari.
 - Mishono Linda boksi
- Shati nyeupe mbili
- Nguo za ndani ni muhimu

- Viatu vyeusi nya ngozi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu pea mbili (2).
- Soksi nyeupe kwa wasichana pea sita (06)
- Sweta mbili rangi ya dark blue

Sare ya michezo: Tracksuit rangi ya dark bluu na raba pea moja kwa jinsia zote.

MAHITAJI YA MWANAFUNZI.

- Daftari (Counter book) kumi na mbili (12)
- Kalam za kuandikia na kucholea na mkebe wa hesabu mmoja.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii ni:-

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inavyotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundu, yenyе dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya waziri mkuu-TAMISEMI yenyе jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kuripoti shulen.

- a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanya kazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d. Kuwahi katika shughuli za shule na zingine utakazopewa.
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g. Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Na
- i. Kutunza mali za Umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-

- a. Wizi
- b. Uasherati na ushoga
- c. Ubakaji

- d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile, uvutaji bangi, Cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e. Kupigana au kupiga
- f. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- g. Kadharau Bendera ya Taifa
- h. Kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha mimba
- i. Kuoa au kuolewa
- j. Kutoa mimba
- k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l. Kukataa adhabu kwa makusudi
- m. Kuwa na simu ya mkononi
- n. Kuingia kwenye baa, majumba ya kulala wageni, kuzurura usiku au kucheza kamari.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulenii na Mwanafunzi.

- a. Medical Examination Fomu, ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shulenii. (imeambatanishwa)
- b. Fomu ya kukubaliana na sheria na kanuni za shule kwa mzazi na mwanafunzi, yenye mkataba kwa Mwanafunzi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (imeambatanishwa)
- c. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

5.0 Tafadhali somo kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA MPESU SEKONDARI

.....
MKUU WA SHULE
0763 873 323

(REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)
THIS FORM IS TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER.

Name of Pupil:.....

Age:..... Sex:.....

The above named has been examined in respect of:

- a) STOOL:.....
- b) URINE (Including UPT for girls).....
- c) CHEST.....
- d) BLOOD:.....
- e) EYES:.....
- f) EARS:.....
- g) OTHER FINDING:.....

.....
.....
.....

I satisfy that the above pupil is **fit/not fit** to pursue further studies in secondary school.

.....
SIGNATURE

.....
DATE

.....
DESIGNATION

.....
STATION

FOMU YA KUKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

a. Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi

Miminimesoma na kuelewa kanuni, sheria za shule, nina ahidi kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.

Sahihi.....Tarehe.....

b. Sehemu hii ijazwe na mzazi

Mimi.....mzazi
Wa.....nimesoma na kuelewa sheria na kanuni za shule, nitatoa ushirikiano kwa walimu katika masuala ya kitaaluma na nidhamu kwa mtoto wangu.

Sahihi.....Tarehe.....

Namba ya simu ya mzazi.....